

Ndugu Alex Tarimo alifanya kazi ya ualimu kwa kufundisha somo la Uchumi kuanzia mwaka 1997 – 2005 katika shule za sekondari za Tegeta (Dar), White Lake (Dar) na Feza (Dar). Aliajiriwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundis kama Afisa Elimu mwaka 2006 na alifanya kazi katika shule za sekondari za Galanos (Tanga) na Pugu (Dar). Mwaka 2007 alihamia Wizara ya Maji kama Mchumi na tangu hapo amepanda madaraja mbalimbali hadi kufikia cheo cha Mchumi Mkuu. Katika Wizara ya Maji anafanya kazi zinazohusu Sera, Mipango, Bajeti pamoja na Ufutiliaji na Tathimini ya miradi.

Bw. Alex alizaliwa katika Wilaya ya Rombo, Mkoani Kilimanjaro mwaka 1969. Alipata Elimu ya Msingi katika Shule ya Msingi Kunduchi, Dar es Salaam (1979 – 1985), Elimu za Sekondari katika Shule za Azania, Dar es Salaam (1986 – 1989) na Ndanda, Mtwara (1990 – 1992). Alipata Shahada ya Uchumi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (1997), Shahada ya Uzamili (MBA) kutoka Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (2008), na Shahada ya Uzamili ya Sayansi katika Uwekezaji (*Msc Investment Management*) kutoka Chuo Kikuu cha Coventry nchini Uingereza (2016). Aidha, ana Stashahada ya Uzamili ya Ualimu (*PGDE*) ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (2011) na mbobezi katika masuala ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binasfi (*Certified Public Private Partnership Specialist*), elimu aliyoipata kutoka Chuo cha Ubia Bainya ya Sekta ya Umma na Sekta Binasfi (*IP3 College*) cha Washington, Marekani.

Aliteuliwa kuwa Kaimu Mkurugenzi Msaidizi katika Idara ya Sera na Mipango Sehemu ya Ufutiliaji na Tathmini mwaka 2019.